



## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (4 MAY 2021).

AKO Group Ltd inayofanya kazi zake hapa Geita Gold Mine (GGM) inakaribisha maombi ya watazania wenye sifa na uwezo wakujiua nafasi kumi (10) zilizo wazi ikumbukwe kwamba wakazi wa maeneo yanayo uzunguka Mgodini wa Geita watapewa kipaumbele kwa kufuata vigezo vilivyowekwa kwa nafasi zifuatazo:-

### **WAHUDUMU NAFASI NNE. (WAITER / WAITRESS)**

#### MAJUKUMU YA WAHUDUMU.

- Kuhumia na kupeleka chakula na vinywaji kwa wageni.
- Kuhakikisha Canteen ni safi na imepangwa vizuri.
- Kufanya Setup ya meza na matayarisho mengine kabla ya muda wa huduma ya chakula kuanza.
- Utekelezaji kwa kiwango cha juu cha huduma kwa wateja ukiwa mgodini
- Kugawa chakula na Vinywaji kwenye shughuli mbalimbali za kiofisi.
- Kufanya majukumu Mengine utakayopangiwa na kiongozi wako.

#### **VICEZO.**

- Elimu kidato cha Nne na kuendelea.
- Cheti katika fani ya Hotelia.

### **WAHUDUMU WA USAFI NAFASI NNE. (HOUSEKEEPING)**

#### MAJUKUMU YA WAHUDUMU WA USAFI.

- Kusafisha vyumba vya wateja na mazingira yake kwa kiwango kinachohitajika na kampuni.
- Utunzaji wa vifaa vyote vya usafi na vya wateja kwa ujumla.
- Utekelezaji kwa kiwango cha juu cha huduma kwa wateja ukiwa mgodini.
- Kuhudhuria vikao vya utendaji kazi kila siku na kwa muda uliopangwa.
- Kutunza Siri za Kampuni.
- Kufuata taarabibu na maelekezo mengine yote utakayopangiwa na kiongozi wako.

#### **VICEZO.**

- Elimu kidato cha Nne na kuendelea.
- Cheti katika fani ya hotelia.



Plot No. 29363, Urafiki Area, Ubungo, PO Box 63314  
Dar Es Salaam, Tanzania



## **DEREVA NAFASI MOJA. (DRIVER)**

### **MAJUKUMU YA DEREVA**

- Kuhakikisha kazi zote zinafanyika kulingana na matakwa ya mteja na Kampuni.
- Kuhakikisha unafuata masharti ya usalama barabarani katika kiwango cha kitaifa na kimataifa.
- Kukagua, kusafisha na kutoa taarifa za ajali au marekebisho ya gari kwa viongozi haraka iwezekanavyo.
- Awe anajua kutumia vizuri vifaa vya usalama pindi awapo kazini.(PPE)
- Kuhudhuria vikao vya utendaji kazi kila siku na kwa muda uliopangwa.
- Kufuata taratibu na maelekezo mengine yote atakayopangiwa na kiongozi wake.

### **VICEZO.**

- Elimu kidato cha nne na kuendelea.
- Cheti cha udereva kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali.
- Leseni ya udereva daraja C,C1, C2,C3, D & E.
- Dereva mwenye ujuzi wa ufundi atapewa kipaombe.

## **KIONGOZI WA DUKA LA VYAKULA NA VITU MBALIMBALI. NAFASI MOJA. (SHOP SUPERVIROR)**

### **MAJUKUMU YA KIONGOZI DUKA LA CHAKULA.**

- Kusimamia mauzo yote ya POS na kutoa Ripoti za kila siku kwa Muhasibu.
- Kuhakikisha mfumo wa Kompyuta (POS) unasimamiwa na kuhakikisha mauzo yote yanapitia katika mfumo huo.
- Kuhakikisha bidhaa zote zinazo hitajika na wateja zinapatikana kwa kushirikiana na wafanyakazi wa stoo na Afisa manunuzi.
- Utoaji wa Ripoti za mauzo ,Ubora wa Bidhaa na Mahesabu ya Bidhaa kila mwezi. (Monthly Stock Count).
- Kufuata taratibu na maelekezo mengine yote atakayopangiwa na kiongozi wake.

### **VICEZO.**

- Diploma in Finance/Accounts/Business Administration.
- Ujuzi wa Kompyuta.
- Uzoefu wa miaka miwili katika fani ya uhasibu atapata kipaombe.

### **UZOEFU UNAOHITAJIKA.**

- Kwa nafasi ya Dereva uzoefu usiopungua miaka mitatu.
- Wahudumu uzoefu usiopungua mwaka mmoja ,ikiwa ni pamoja na kufahamu mambo yote muhimu katika fani husika.
- Awe anafahamu kusoma na kuandika.(Kiingereza ni muhimu zaidi)
- Uzoefu wa kufanya kazi katika hoteli yenye hadhi ya nyota tano atapewa kipaombe.

+255 22 700 646

info@akogroup.co.tz

www.akogroup.co.tz

Plot No. 29363, Urafiki Area, Linyolimo 1, Box 333 In Dar Es Salaam, Tanzania






### ANGALIZO

- Barua za maombi ziambatanishwe na barua ya utambulisho kutoka ofisi ya mwenyekiti wa kitongoji au kijiji husika.
- Epuka matapeli wanaotumia fursa hii kujifanya maafisa waajiri wa AKO Group Ltd.
- AKO Group Ltd haifanyi usaili/interview kwa njia ya simu. ( tafadhari toa taarifa kwa uongozi endapo utapigiwa simu na kuombwa pesa kusaidiwa kupata kazi.)
- Hakikisha umeandika vizuri NAFASI unayo omba kwenye barua yako.
- Barua ziandikwe na kupelekwa Geti la Mike One pamoja na Geti la Nyakabale (Mike One Alpha) kwa anuani ya AKO GROUP LTD, GEITA GOLD MINE BOX 63314. AU kwa Barua pepe [rmashinga@akogroup.co.tz](mailto:rmashinga@akogroup.co.tz)
- Tarehe ya mwisho kutuma maombi ni tarehe 17 May 2021 saa 11:00 jioni.

Kama hujapigiwa simu na Ofisi ya AKO ndani ya siku 5 baada ya siku ya mwisho ya kupokea maombi, basi ujue ombi lako halikufanikiwa ujaribu tena wakati mwingine.

Mafanikio Mema,  
AKO Group Ltd

  
Meneja Rasimwa

